Jibu: Turejee,

> *Mithali 25:12 “KIPULI CHA DHAHABU, na pambo la dhahabu safi; Ndivyo alivyo mwonyaji mwenye hekima kwa sikio lisikialo”*

“Kipuli” ni jina lingine la “hereni za masikioni”.

Neno hili limeonekana mara moja tu katika biblia, katika kitabu cha *Mithali 25:12.*

Na mwandishi wa Mithali *(Sulemani)* kwa hekima ya roho alipata kuelewa vipuli *(hereni)* sahihi wanazopaswa wavae watu, tofauti na hizi tuzijuazo.

Anasema… *“KIPULI CHA DHAHABU, na pambo la dhahabu safi; Ndivyo alivyo MWONYAJI MWENYE HEKIMA KWA SIKIO LISIKIALO”.*

Maana yake ni kuwa sikio linalosikia hekima kutoka kwa wenye hekima, linafananishwa na sikio lililovishwa hereni ya dhahabu au pambo la dhahabu.

Kwa lugha nyingine ni kwamba, kama tukitaka kupamba masikio yetu kwa vitu vya thamani, basi tuwe wasikilizaji wa maneno ya hekima. *(Kwani maneno hayo yataonekana kama mapambo ya thamani katika masikio yetu).*

Na maneno ya hekima hatuyapati pengine isipokuwa katika biblia takatifu *(Humo ndimo tutakapopata lulu na mapambo ya thamani ya masikio yetu)..*

> *Mithali 2:1 “Mwanangu, kama ukiyakubali maneno yangu, Na kuyaweka akiba maagizo yangu;*

> *2 HATA UKATEGA SIKIO LAKO KUSIKIA HEKIMA, UKAUELEKEZA MOYO WAKO UPATE KUFAHAMU;*

> *3 Naam, ukiita busara, Na kupaza sauti yako upate ufahamu;*

> *4 Ukiutafuta kama fedha, Na kuutafutia kama hazina iliyositirika;*

> *5 Ndipo utakapofahamu kumcha Bwana, Na kupata kumjua Mungu”*

Soma tena Mithali 4:20, Mithali 5:1, na Mithali 22:17 utaona maneno yanayopatana na hayo..

Mithali hizi zinalingana kabisa na ujumbe wa Roho Mtakatifu tunaousoma katika kitabu cha *1Petro 3:3. Na 1 Timotheo 2:9.*

> *1 Petro 3:3 “Kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi;*

> *4 BALI KUWE UTU WA MOYONI USIOONEKANA, KATIKA*

> *MAPAMBO YASIYOHARIBIKA; YAANI, ROHO YA UPOLE NA UTULIVU, ILIYO YA THAMANI KUU MBELE ZA MUNGU.*

> *5 Maana hivyo ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu, na kuwatii waume zao.*

> *6 Kama vile Sara alivyomtii Ibrahimu, akamwita Bwana; nanyi ni watoto wake, mfanyapo mema, wala hamkutishwa kwa hofu yo yote”.*

Mstari wa 4 unasema... “ *BALI KUWE UTU WA MOYONI USIOONEKANA, KATIKA MAPAMBO YASIYOHARIBIKA; YAANI, ROHO YA UPOLE NA UTULIVU, ILIYO YA THAMANI KUU MBELE ZA MUNGU”.*

Je ni vipuli gani vipo masikioni mwako?...vya chuma au vya maneno ya hekima?.

Bwana atusaidie.

Shalom.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia unaweza ukapata mafundisho haya Kwa njia ya Whatsapp yako, jiunge na channel yetu Kwa kubofya hapa >> WHATSAPP

Mafundisho mengine:

Rudi nyumbani

Share on:
WhatsApp